

## CHELSEA 🇬🇧

by STANLEY KIYONDI

Imenilazimu kukiri, yote yaliyo moyoni,  
Penzi langu meghairi, menitonesha dondani,  
Sio pekee fikiri, Mashabiki kilioni,  
Iko wapi ya zamani, Chelsea yenyе furaha?


Tumbo limejaa maji, Najutia kushabiki,  
Kadhani kipo kipaji, Lo! Kichapo  
kila wiki,  
Kunyamaa ja friji, Wenzetu wao  
mikiki,  
Iko wapi ya zamani, Chelsea yenyе  
furaha?

Kila kukija miradi, Ni ile ya kusajili,  
Mikataba tia midadi, Kikosi kuwa  
kikali,  
Kumbe Kaleta baridi, Timu ipo chini  
Chali,  
Chombo sasa hakiendi, Naomba  
mbinu badili,

Nyeusi suti valia, Wamiliki na  
meneja,  
Mshahara kupokea, Kutimiza zenu  
haja,  
Huna haja kupakia, Pakacha  
limeshavuja  
Mkiani kasalia, Nani wa  
kutupambaja?

Kumi na moja nafasi, jedwalini  
shikamana  
UEFA hatuna tetesi, Kwa mbali  
tumepakana,  
Benzema kaja kwa kasi, kepa naye  
kachana mbuga  
Ewe Masiya naomba, Fariji wana Chelsea!

Dau kubwa duniani, Kina Modryk Kaleta,



Enzo Fofana tuani, Sterling hamkusita,  
Kushinda mkaplani, Kumbe miguu ya bata,  
Hawezi fuma golini, Katwacha tukila mwata!

Kimetanda cha kaniki, Stamford hapakaliki,  
Hasidi hawashikiki, Kutuchapa hawatosheki,  
Mwendo punguza breki, kwani sisi hatushuki,  
Iko wapi ya zamani, CHELSEA yenyeye furaha?

Punda sasa amechoka, miguu kutapatapa,  
Ukingoni tumefika, maji shingoni kukapa,  
Hana nguvu kuinuka, wala mja kumlipa,  
Wenyewe Msiba kataka, Na sasa hatwezi kwepa.